JARIDA LA

# TANDAHIMBA

Jarida la mwezi Machi, 2025 | www.tandahimbadc.go.tz

## 4 MINNE YA NGUVU YA RAIS SAMIA TANDAHIMBA

Haliuzwi



1. SEKTA YA ELIMU
2. SEKTA YA AFYA
3. SEKTA YA KILIMO MIFUGO NA UVUVI
4. MAENDELEO YA JAMII
5. SEKTA YA MAJI
6. SEKTA YA BARABARA

*"Tandahimba tumejipanga, kazi zinaendelea"*

# UTANGULIZI



**Mhe.Baisa Baisa**
**Mwenyekiti wa Halmashauri**
**ya Wilaya ya Tandahimba**



**DCI.Mariam Mwanzalima**
**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri**
**ya Wilaya ya Tandahimba**

Ni miaka minne tangu kuapishwa kwa Rais wa awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt Samia Suluhu Hassan Machi 19,2021.Ambapo ameendeleza gurudumu la Maendeleo katika sekta mbalimba Nchini akiimarisha Diplomasia na mataifa mbalimbali hali ambayo imepelekea mapinduzi makubwa ya kiuchumi.

Aidha,Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ni miongoni mwa Wilaya tano zilizopo katika Mkoa wa Mtwara ambayo ni wanufaika wa Maendeleo katika sekta mbalimbali baada ya kupokea fedha za utekelezaji wa miradi mikubwa ya Maendeleo katika Serikali ya Awamu ya sita

Katika Jarida hili toleo maalumu limeangazia maendeleo na mafanikio yaliyofikiwa kwa kipindi cha miaka minne kwenye Sekta mbalimbali ikiwemo Elimu, Afya, Maji na miundombinu ya barabara na mengine mengi.

# 1 SEKTA YA ELIMU

## Elimu ya Awali na Msingi

Halmashauri ya Wilaya Tandahimba, ina shule za Msingi 133, zenye jumla ya wanafunzi 59,850 wakijumuishwa wanafunzi wa Elimu ya Awali na Elimu maalum Halmashauri ina jumla ya walimu 917.



Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kipindi cha miaka minne ya Uongozi jumla ya fedha Tsh.Bilioni 1.26 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 32 yenye thamani ya Tsh.Milioni 438 matundu ya vyoo 306 yenye thamani ya Tsh.Milioni 532 , uchimbaji wa kisima na ujenzi wa miundombinu ya uvunaji maji na sehemu ya kunawia mikono katika Shule za Msingi 131.



# DONDOO MUHIMU ZA MAFANIKIO BAADA YA UBORESHAJI WA ELIMU YA AWALI NA MSINGI

1. Uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza umeongezeka kutoka wanafunzi 7428 mwaka 2022 hadi wanafunzi 7697 mwaka 2025 huku ufaulu wa darasa la nne ukiongezeka na kufikia asilimia 93 sambamba na darasa la saba ufaulu ukiongezeka na kufikia asilimia 80 mwaka 2024.

2. Katika kipindi cha miaka minne jumla ya nyumba 9 za walimu zimeongezeka zenye thamani ya Tsh. Milioni 295 na miundombinu ya maji imejengwa yenye thamani ya Tsh.Milioni 35.

3. Kuongezeka kwa shule Elimu ya Awali na Msingi kutoka shule 127 Mwaka 2021 hadi shule 133 Mwaka 2025




***Moja ya madarasa katika Shule mpya ya Msingi Mambamba iliyojengwa kwa Tsh Milioni 331.6 fedha kutoka Serikali kuu katika kipindi cha Miaka Minne ya Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan***

# Elimu Sekondari



Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ina shule za sekondari 32 ambazo zinawanafunzi 14,708 katika shule za sekondari wakiwemo wavulana 6754 na wasichana 7954 sambamba na walimu 403 wanaofundisha masomo ya sayansi, sanaa, biashara na kilimo .

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ina shule 3 za sekondari zinazotoa elimu ya kidato cha tano na sita ambazo ni Tandahimba, Kitama, na Nandonde.

Serikali ya awamu ya Sita chini ya Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imeendelea kuboresha Sekta ya Elimu kwa kuboresha miundombinu ya madarasa, maabara za kujifunzia,nyumba za walimu, kuongeza ajira za walimu pamoja na kutoa Elimu bila malipo(kidato cha kwanza hadi cha sita).

Katika kipindi cha Miaka minne ya Rais Dkt.Samia madarakani jumla ya kiasi cha Tsh.Bilioni 6.76 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Elimu ikiwemo madarasa, Vyoo, Nyumba za Walimu, kugha



ramia elimu bila malipo na chakula kwa wanafunzi wa Bweni. .

Aidha, miradi ya Elimu Sekondari iliyotekelezwa ni Ujenzi wa madarasa 91 , Ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 10 katika shule saba (7) , Maabara 13, mabweni 8, ujenzi wa nyumba 2 za walimu , Ujenzi wa Shule mpya 4 za Sekondari

# DONDOO MUHIMU ZA MAFANIKIO BAADA YA UBORESHAJI WA ELIMU SEKONDARI WILAYA YA TANDAHIMBA



*Shule Mpya ya Sekondari Makondeni iliyogharimu Tsh.Milioni 470 fedha kutoka Serikali kuu kupitia mradi wa SEQUIP*

1. Kuongeza nafasi na fursa za wanafunzi kupata elimu ya Sekondari katika mazingira yao. Kwa ujenzi wa shule 4 za sekondari wanafunzi zaidi ya 1,600 watapata nafasi katika shule hizo.

2. Ufaulu wa mitihani ya kitaifa ya Kidato cha Nne umeongezeka kutoka asilimia 87 mwaka 2021 hadi asilimia 96 mwaka 2024.

3. Ufaulu wa Mtihani wa Taifa wa kidato cha Sita umeendelea kuwa ni uleule wa asilimia 100 kwa miaka yote minne ila katika ufaulu wa juu zaidi

4. Ujenzi wa shule mpya na miundominu umesaidia kupunguza umbali wa wanafunzi kutembea kutoka nyumbani kwenda shuleni hivyo kuongeza ufani-





# 2 SEKTA YA AFYA



**Serikali imetoa kiasi cha Tsh.Milioni 446.4 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Maheha ambapo majengo Manne ikiwemo Jengo la Wagonjwa wa Nje(OPD), Jengo la kujifungulia na Upasuaji pamoja na kichomea taka vimejengwa.**

Halmashauri ina jumla ya vituo 46 vya kutolea huduma za Afya. Katika vituo hivyo kuna Hospitali 1 vituo vya Afya 9 , Zahanati 36 .

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Samia jumla ya Tsh.Bilioni 8.12 zimetolewa kwa ajili ya kuboresha huduma za Afya katika vituo vya kutolea huduma za Afya Ikiwemo Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati.

Aidha jumla ya zahanati mpya tatu ikiwemo Miuta, Dinduma na Mnazi Mmoja zimefunguliwa na jumla ya Vituo vya Afya vitano vimefunguliwa ambavyo vilipandishwa hadhi kutoka zahanati hadi Vituo vya Afya ikiwemo Maheha, Kitama, Litehu, Mambamba na Mihambwe.

Jumla ya zahanati nane zimefanyiwa ukarabati wa vyumba vya kujifungulia kina mama ikiwemo kujengewa vyoo vya ndani, ujenzi wa vyoo vya wagonjwa na watumishi, ujenzi wa vichomea taka na uwekaji wa miundombinu ya maji safi na maji taka .

Katika kipindi Cha miaka minne Serikali imetoa kiasi cha Tsh. Bilioni 1.75 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba vya Hospitali,vituo vya afya na zahanati hali ambayo imepelekea wananchi kupata kuduma za afya bora .



# DONDOO MUHIMU KATIKA SEKTA YA AFYA



1. Uwepo wa dawa (Essential Medicine) umeongezeka kutoka 88% hadi 93%.

2. Vituo vyote vinapatiwa dawa, vitendanishi vya maabara na vifaa tiba

3. Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imetoa mashine mbalimbali kutoka Serikalini kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ikwemo X-ray Mashine,Mashine ya kuchomea taka, Mashine ya kufulia nguo, Mashine ya kutengenezea mifuko ya kuwekea taka na Pasi ya kunyoshea

4. Katika kupambana na malaria jumla ya Wajawazito 31,664 na watoto 35,879 wamepewa vyandarua bure.

5. Jumla ya wajawazito 87,779 kati ya 93,807 sawa na 93.6% wamepatiwa vidonge vya kuongeza wingi wa damu.

6. Katika kipindi cha miaka minne Serikali ya awamu ya sita imetoa magari 3 kwa ajili ya kubebea wagonnjwa na moja kwa ajili ya shughuli za kiutawala na kufanya jumla ya magari 7 na pikipiki 22 katika Idara ya Afya.

7. Katika kipindi cha miaka minne Serikali ya awamu ya sita imetoa fedha kiasi cha Tsh.Milioni 302 kwa ajili ya ujenzi wa Nyumba 8 za wa watumishi wa Afya kwenye Hospitali, vituo vya Afya na Zahanati na kuongeza idadi kutoka nyumba 85 hadi nyumba 93 mwaka 2025.

# 3 SEKTA YA KILIMO MIFUGO NA UVUVI

Katika kuboresha sekta ya kilimo Serikali chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa Pembejeo zenye Ruzuku mifuko 637,507 ya Salfa na lita 127,343 kwa ajili ya kupulizia mikorosho ambapo kuwepo kwa pembejeo hizo kumefufua na kuboresha uzalishaji wa zao la korosho ambalo ndio uti wa Mgongo wa uchumi wa Tandahimba.

katika kukusanya ushuru na kuongeza mapato ya Halmashauri.

Katika hatua Nyingine Serikali ya Dkt.Samia Suluhu Hassan imefanikiwa kutoa vyombo vya usafiri kwa maafisa ugani wa kilimo na mifugo ambapo jumla

ya pikipiki 72 zilipokelewa na kugawiwa kwa Maafisa hao ambapo zimesaidia kurahisisha ufikaji wa maeneo yao



Aidha, mauzo ya wakulima yamekuwa salama kwa kuuzwa kupitia mfumo wa stakabdhi ghalani hali inayoong za pia ufanisi wa Halmashauri ya kazi na kuwahudumia wananchi kwa wakati.

## UVUVI

Serikali katika Sekta ya Uvuvi Serikali ya Rais Samia imetoa



kiasi cha Tsh. Milioni 128 kwa ajili ya wa ujenzi wa mradi wa shamba darasa la ufugaji viumbe maji. Mradi huu unatekelezwa katika kijiji cha Chaume kata ya chaume Tarafa ya Litehu,

Miundombinu iliyopangwa kujengwa ni mabwawa manne, jengo la kufundishia, Ofisi, vyoo vya matundu mawili na Uzio ambapo

# DONDOO MUHIMU KATIKA SEKTA YA KILIMO, MIFUGO KWA KPINDI CHA MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA MADARAKANI



1. Kuongezeka kwa uzalishaji kutakakopelekea Wilaya kuwa na usalama wa chakula pamoja na kukua kwa biashara ya mazao ya chakula kutokana na ziada itakayo zalishwa.

2. Kipato cha mtu mmojammoja pamoja na ushuru wa Serikali vinaendelea kuongezeka kutokana na makusanyo ya zao la korosho, Ufuta na Mbaazi.

3. Katika Ushirika mazao yanayosimamiwa na ushirika yanaendelea kuimarika na masoko yake ni ya uhakika.

4. Pikipiki zilizotolwa na Serikali zimewawezesha maafisa ugani wa kilimo na mifugo kuwafikia wakulima na wafugaji kwa urahisi zaidi hivyo kuongeza tija kwenye shughuli za kilimo na ufugaji.

# 4 MAENDELEOYA JAMII

Katika kipindi cha miaka minne chini ya uongozi wa Dr. Samia Suluhu Hassani Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imeweza kutoa Mikopo isiyo na riba kupitia mapato ya ndani ambapo jumla ya Tsh. Bilioni 1.7 imetolewa kwa Vikundi 163 vya Wanawake, Vijana na watu wenye Ulemavu vyenye jumla ya wanachama 830 kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kupitia vikundi vya ujasariamali .

> ***" Mikopo hii imesaidia kutoa jumla ya ajira 1,304 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kutumia fursa zilizopo katika sekta za ufundi, kilimo, usafirishaji na biashara ndogo ndogo".***




Bwana Muhib Hatib Nahama mkazi wa Tandahimba na Mjasiriamali mwenye ulemavu amenufaika na mkopo wa asilimia kumi wa halmashauri kiasi cha shilingi milioni 8 zilizomuwezesha kufungua kiwanda kidogo cha kutengeneza viatu vya ngozi na shanga ambapo shilingi milioni 6 zilitumika kununulia mashine mbalimbali za ushinaji na shilingi milioni 2 kwa ajili ya malighafi

Aloyce Massau Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii Tandahimba.

Picha hapo chini , ni mtu mwenye ulemavu akifurahia shughuli zake za utengenezaji viatu kutokana na kuwezeshwa mkopo toka Halmashauri ya Tandahimba.

## TASAF

Katika kipindi cha Miaka minne Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF) imetoa kiasi cha fedha Shilingi Bilioni 9.2 kwa kwa ajili ya kuwafikia walengwa wa kaya masikini zipatazo 10,056 katika vijiji 157 sambamba na kuwezesha shughuli za Miradi ya Ajira ya Muda (PWP) .

# DONDOO MUHIMU ZA SHUGHULI ZA TASAF



1. Kupitia TASAF jumla ya Shilingi Milioni 708.2 zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza miradi 406 ambayo ni visima vya kuvunia maji ya mvua 215, barabara za jamii 150, miti ya matunda 39 usambazaji wa miundombinu ya maji miradi 2

2. Walengwa 1,126 wamepewa shiligi 394,100,000 kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza shughuli za kiuchumi ili kukuza kipato cha Kaya katika vijiji 88, ambapo kila mlengwa amepata shilingi 350,000.

3. Walengwa 6,012 wamepata ujuzi na maarifa wa ujenzi wa visima vya kuvunia maji ya mvua, upandaji miti ya matunda na ujenzi wa barabara

4. Kuimarika kwa shughuli za usafirishaji kutokana na utekelezaji wa miradi ya barabara za jamii 150.

5. Walengwa 1,126 wamepata ruzuku kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza shughuli za kiuchumi ili kuinua kipato cha kaya.

6. Asilimia 100 ya watoto chini ya miaka mitano wanapelekwa kliniki na 97% ya wanafunzi kutoka kaya za walengwa wanahudhuria shulen



Hadija Nyalaka Mkazi wa Kijiji cha Shangani –Mchichira akiwa kwenye biashara yake ya ubanguaji korosho

# 5 SEKTA YA MAJI




## MAMLAKA YA MAJI MAKODE

Mamlaka ya maji makonde imetekeleza miradi ya maji mjini katika Halamashauri ya Wilaya ya Tandahimba ambapo katika mkipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita imetekeleza Miradi ya maji mitatu yenye thamani ya Shilingi Bilioni 101.9 katika Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba na kuwanufaisha zaidi ya wakazi 330,0000 wananufaika na miradi hiyo

Mradi wa maji Makonde unaogharimu Shilingi Bilioni 84.7 unaojengwa katika kata ya Namikupa unaendelea kutelezwa ambapo unatarajia kuwanufaisha wakazi wapatao 330,000.

Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Tandahimba imetekeleza miradi ya maji 13 yenye thamani ya Tsh Bilioni 18.13 ambapo itahudumia watu wapatao 126,193 ambayo kati ya miradi hiyo miradi 8 imekamilika na kutoa huduma ya maji safi na salama ambapo hapo awali hali ya upatikanaji wa huduma ya maji ilikuwa asilimia 48 hadi sasa ni asilimia



# DONDOO MUHIMU SEKTA YA MAJI KWA MIAKA MINNE YA UONGOZI WA RAIS SAMIA



i) Hali ya upatikanaji wa maji imeongezeka kutoka 48% ya awali na kufikia 60% ambapo kuna miradi mikubwa inaendelea utekelezaji na inategemea kukamilika mwezi Desemba 2025 ambapo kukamilika kwake kutaongeza asilimia 28.8 na kufanya jumla ya 88.8% ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa Wilaya ya Tandahimba

ii) Mradi wa Maji Mkwiti Lot 3 umetekelezwa kwa mwaka fedha 2021/2022 wenye gharama ya Tsh Bilioni 6.5 unahudumia vijiji 16 vya Mkwiti Juu, Mkwiti Chini, Mangombya,Nanjanga,Nannala,Chidede, Luagala, Michinji, Kigamboni, Mkuti,Mkola Chini, Mkola Juu, Namindondi Juu, Namindondi Chini, Mabeti, Ngunja, Mmeda, Libobe na Litehu sawa na watu wapatao 26,164 ambapo mradi huu upo hatua ya majaribio ya maji sawa na asilimia 90 ya utekelezaji ambapo hadi sasa Vijiji 11 tayari vimeshaanza kupata huduma ya maji safi na salama.Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza asilimia 4.7 ya upatikanaji wa huduma ya maji kiwilaya.



iv) Mradi wa Maji Chitoholi-Lubangala umetekelezwa kwa mwaka fedha 2023/2024 wenye gharama ya Tsh Bilioni 1.4 ambapo chanzo cha fedha ni P4R unahudumia wananchi wapatao 10,817 katika vijiji 6 vya Chitoholi Juu,Chitoholi Shuleni, Mikunda Shuleni, Mikunda Sokoni, Dinembo na Lubangala wanapata huduma ya maji safi na salama ambapo pia umeongeza asilimia 4 ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa ngazi ya Wilaya.

v) Mradi wa Maji Mitondi A & B umetekelezwa kwa mwaka fedha 2023/2024 huu wenye gharama ya Tsh Milioni 792.2 ambapo chanzo cha fedha ni PforR unahudumia wananchi 4025 katika vijiji 2 vya Mitondi A na Mitondi B ambapo wanapata huduma ya maji safi na salama mradi huu umekamilika mwaka 2024.Kumeongeza asilimia 1.3 ya upatikanaji wa huduma ya maji kiwilaya.



vi) Mradi Maji Mkwiti Lot 3 umetekelezwa kwa mwaka fedha 2021/2022 huu wenye gharama ya Tsh Bilioni 6,537,327,499.5 ambapo unahudumia vijiji 16 vya Mkwiti Juu, Mkwiti Chini, Mangombya,Nanjanga,Nannala,Chidede, Luagala, Michinji, Kigamboni, Mkuti,Mkola Chini, Mkola Juu, Namindondi Juu, Namindondi Chini, Mabeti, Ngunja, Mmeda, Libobe na Litehu sawa watu wapatao 26,164 na mradi huu upo ya majaribio ya maji ambapo sawa na asilimia 90 ya utekelezaji ambapo hadi sasa Vijiji 11 tayari vimeshaanza kupata huduma ya maji safi na salama.Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza asilimia 4.7 ya upatikanaji wa huduma ya maji

# 6 SEKTA YA BARABARA




Wakala wa barabara za Vijijini na Mijini TARURA Wilaya ya Tandahimba inahudumia mtandao wa barabara wenye urefu wa Kilomita 974.55 ambapo mwaka 2021 bajeti ya TARURA Wilaya ya Tandahimba ilikuwa Tshs.Bilioni 1.08 na katika kipindi cha miaka mine ya Uongozi wa Rais Samia Bajeti imeongezeka na kufikia ni Tshs. Bilioni 2.58 sawa na ongezeko la 58.11% kwa mwaka.

Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt.Samia imetoa kiasi cha Tsh Bilioni 9.7 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundondimbu ya barabara wenye tija Wilaya ya Tandahimba

Matengenezo ya barabara kwa kiwango cha lami na ufungaji wa Taa wastani wa kilomita 10.3 yamefanyika na kugharimu kiasi cha Tsh.Bilioni 5.22 fedha kutoka Serikali kuu.

Aidha, Seikali katika kipindi cha miaka Minne ya uongozi wa Rais Samia Sluhu Hassan imetoa kiasi cha Tsh. Bilioni 1.6 kwa ajili ya utengenezaji wa barabara katika sehemu korofi zenye wastani wa kilomita 220.05 .ukarabati wa miundondimbu ya barabara wenye tija Wilaya ya Tandahimba Matengenezo ya barabara kwa kiwango cha lami na ufungaji wa Taa wastani wa kilomita 10.3 yamefanyika na kugharimu kiasi cha Tsh.Bilioni 5.22 fedha kutoka Serikali kuu.

Aidha, Seikali katika kipindi cha miaka Minne ya uongozi wa Rais Samia Sluhu Hassan imetoa kiasi cha Tsh. Bilioni 1.6 kwa ajili ya utengenezaji wa barabara katika sehemu korofi zenye wastani wa kilomita 220.05 .

# VIONGOZI WA KITAIFA WALIOFANYA ZIARA KATIKA HALMASHAURIYA WILAYA YA TANDAHIMBA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Mnamo Septemba 16, 2023 alizungumza na wananchi kupitia Mkutano wa hadhara katika uwanja wa Majaliwa ambapo katika ziara hiyo Rais Samia aliambatana na Mawaziri kadhaa akiwemo Waziri wa Kilimo Mhe.Hussein Bashe, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Mohamed Mchengerwa sambamba na viongozi wengine wa kitaifa.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Agosti 13, 2023 alifanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo na kuzungumza na wananchi kata ya Kitama na Mndumbwe Wilaya ya Tandahimba.



Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mhe. Stergomena Tax Oktoba 7, 2024 alizindua mradi wa maji Chitoholi na kuzungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwnja wa Forodhani



Aliyekuwa Naibu waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mhe.-David Silinde Desemba 5, 2023 alipokuja kuzindua mfumo wa upimaji wa Mazao kupitia mizani ya kidigitali kwenye Maghala ya Chama Kikuu cha Ushirika(TANECU)



Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt.Grace Magembe Julai 27, 2022 alitembelea Miradi ya Afya ikiwemo kituo cha Afya Maheha na Nyumba za watumishi.



Mwenyekiti wa UWT Mary Chatanda Julai 20, 2023 kukagua miradi ya maendeleo na kuzungumza na wananchi katika kata ya Mdimba na Mndumbwe.

# WAGENI MBALIMBALI WALIOKUJA KUJIFUNZA UZALISHAJI BORA WA ZAO LAKOROSHO, UUZAJI KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI GHALANI NA UENDESHAJI BORA WA MFUKO WA ELIMU HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA .



Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ni kinara wa Uzalishaji wa korosho zenye ubora Nchini Tanzania ambapo zaidi ya Asilimia 90 ya Uchumi wa wananchi wa Tandahimba unategemea zao hilo.Aidha,Serikali ya awamu ya Sita katika kipindi cha miaka Minne imeboresha zao hilo kwa kutoa pembejeo Zaidi ya 500,000 na viuatilifu kwa wakulima hali iliyopelekea uzalishaji kuongezeka. Sambamba na hilo Wilaya ya Tandahimba inakusanya ushuru utokanao na korosho kupitia Mfumo wa Stakabadhi ghalani ambao umekuwa na ufanisi na kuvutia wageni kutoka maeneo mbalimbali kuja kujifunza.Baadhi ya wageni kutoka Maeneo mbalimbali Nchini waliokuja kujifunza ni pamoja na;

# BAADHI YA WAGENI KUTOKA MAENEO MBALIMBALI NCHINI WALIOKUJA KUJIFUNZA UZALISHAJI BORA WA KOROSHO, MFUMO WA STAKABADHI GHALANI NA MFUKO WA ELIMU



## HALMASHAURI YA WILAYA YA MALINYI

Baraza la Madiwani na wataalamu walifanya ziara ya kujifunza uuzaji wa mazao kwa nia ya Mfumo wa Stakabdhi ghalani Februari 28, 2023.




## HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

Baraza la madiwani na Wataalamu Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji walifanya Ziara Tandahimba na kujifunza Jninsi Mfumo wa Stakabadhi Ghalani unavy-ofanya kazi kwa wakulima wa Korosho Julai 13, 2023.



## HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

Desemba 14, 2023 Baraza la madi-wani, Wakuu wa Idara wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe wali-kuja kujifunza Tandahimba uzalishaji wa kilimo bora cha Korosho.




## ALAT MKOA WA SONGWE

Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania(ALAT) na wataalamu Mkoa wa Songwe walikuja kujifunza namna bora ya uendeshaji wa Mfuko wa Elimu Julai 2, 2024



## HALMASHURI YA WILAYA YA TUNDURU.

Baraza la madiwani Mbunge na Wataalamu wa Halmashuri ya Wilaya ya Tunduru walifanya ziara ya kujifunza uzalishaji wa Zao la Korosho na uuzaji wa mazao mengine kupitia Mfumo wa Stakabadhi ghalani Machi 4, 2024



## HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA

Baraza la Madiwani na Wataalamu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Siha Mkoani Kilimanjaro walipokuja kujifunza namna bora ya Ukusanyaji bora wa Mapato kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani sambamba na uendeshaji wa Mfuko wa Elimu Agosti 1, 2024



## CHUO CHA TAIFA CHA ULINZI TANZANIA

Wakufunzi na wanafunzi wa Chuo cha Taifa Ulinzi Tanzania(NDC) walikuja kujifunza uzalshaji bora wa zao korosho Januari 16, 2025



# Contacts

Tandahimba District Council-TDC

tandahimbadistrictcouncil

www.tandahimbadc.go.tz

TDC ONLINE TV

*Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*
*Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba*